Je, upatikanaji wa umeme unaathiri vipi raia nchini Kenya?

Katika muongo mmoja uliopita, upatikanaji wa umeme nchini Kenya umeongezeka kwa kasi. Matokeo yake, kwa sasa ina moja ya viwango vya juu zaidi vya upatikanaji wa umeme barani Afrika. Hata hivyo, kwa sababu ya gharama kubwa na upatikanaji usio wa uhakika, kaya nyingi zinaendelea kupata shida kukidhi mahitaji yao ya kila siku ya nishati. Timu ya watafiti kutoka Kenya, Kanada na Marekani inachunguza athari za kiuchumi, kijamii na kisiasa za upatikanaji wa umeme. Utafiti wao unachunguza kwa namna gani ubora na wingi wa umeme unavyoathiri kaya, pamoja na changamoto katika kusambaza umeme kwa usawa kote nchini Kenya.

Washiriki wa timu
Dkt Elizabeth Baldwin
Dkt Jennifer Brass
Dkt Christopher Gore
Dkt Lauren MacLean
Dkt Winnie Mitullah
Dkt Alesha Porisky

Nyanja za utafiti
Sayansi ya siasa, sera ya umma, masomo ya mazingira

Mradi wa utafiti
Kuchunguza athari za kijamii, kiuchumi na kisiasa za upatikanaji wa umeme nchini Kenya

Mfadhili
Baraza la Utafiti wa Sayansi ya Jamii na Binadamu la Kanada (SSHRC)

Faharasa

Kuzima — Umeme kukatika

Haki ya Nishati — upatikanaji sawa wa umeme wa kuaminika na wa bei nafuu kwa wotel

Gridi — mtandao wa kitaifa wa miundombinu ambayo inatoa umeme kwa watumiaji

Mafuta ya taa — mafuta ya kimiminika, ambayo hutumika kwa kawaida kuwasha taa katika nchi nyingi za kipato cha chini barani Afrika

Ushiriki wa Kisiasa — kushiriki katika shughuli zozote zinazohusiana na siasa, kama vile kupiga kura, kampeni, kuhudhuria mikutano na kujadili siasa

Wengi wetu tunachukulia umeme kama kitu cha kawaida. Ikiwa tunataka kuwasha taa au kutazama TV, tunaponyeza tu swichi. Ikiwa tunahitaji kuchaji simu zetu, tunachomeka tu. Lakini kwa mamilioni ya watu duniani kote, umeme ni ghali, sio wa uhakika au hata haupo kabisa.

Upatikanaji wa umeme nchini Kenya

Timu ya kimataifa ya watafiti inachunguza athari za upatikanaji wa umeme nchini Kenya. Ikiwa ni mojawapo ya nchi yenye viwango vya juu zaidi vya upatikanaji wa umeme barani Afrika, Kenya inasifiwa kama hadithi ya mafanikio. “Asilimia ya kaya zinazopata umeme imeongezeka karibia mara mbili katika kipindi cha miaka 10 iliyopita - kutoka karibu 40% mwaka 2015 hadi karibu 80% mwaka 2025,” anaelezea Jennifer.

Na Kenya pia inaongoza katika nishati ya kijani, na zaidi ya 90% ya umeme huu unatoka kwa vyanzo mbadala, hasa nishati ya jotoardhi na ya maji. Kwa kuzingatia athari mbaya ya mazingira ya nishati ya mafuta ya kale, haya ni maendeleo ya kupongezwa.

“Ingawa Kenya inapaswa kupongezwa kwa maendeleo haya, ni muhimu kutambua kwamba ‘upatikanaji’ haimaanishi upatikanaji wa gridi ya umeme,” anasema Elizabeth. Kama Christopher anavyoeleza, “Nchini Kenya, takwimu za kitaifa hazitofautishi waziwazi kati ya mtu mwenye paneli ndogo ya jua inayowasha balbu moja na mtu ambaye nyumba yake imeunganishwa kwenye gridi ya taifa na ambaye ana jiko la umeme la kupikia, friji na TV.”

“Ingawa asilimia kubwa ya kaya na wafanyabiashara wanaweza kupata umeme kinadharia, kiutendaji, usambazaji sio wa kawaida (kukatika ni jambo la kawaida) na watu wengi hawawezi kumudu gharama ya kufunga au kutumia umeme,” anaelezea Winnie. Hii ina maanisha kuwa Wakenya wengi wana uwezo mdogo wa kutumia umeme nyumbani na kazini. “Hii inawafanya watu wahisi kama wanasiasa na watunga sera wana shindwa katika ahadi yao ya kusambaza umeme kwa wote,” anasema Jennifer.

Kuchunguza zaidi

Ili kuelewa zaidi kuhusu athari za kupata umeme, timu ilishirikiana na kampuni ya utafiti wa kijamii ya Kenya, TIFA Research Kenya, kutoa mafunzo

Kituo cha biashara cha mashambani cha Kenya chenye umeme

kwa watafiti wasaidizi wa ndani kufanya tafiti za kaya na kuajiri washiriki kwa utafiti wa makundi. Tafiti ziliuliza maswali kama vile ikiwa nyumba ina umeme, unatoka wapi (k.m., gridi ya taifa au sola), usambazaji huo unategemewa kiasi gani, wanatumia kiasi gani cha umeme, gharama yake ni kiasi gani, wanamiliki vifaa vingapi vinavyotumia umeme, na iwapo na jinsi gani wakaaji wanaendesha biashara na kushiriki katika shughuli za kijamii na kisiasa. “Maswali haya yalituruhusu kupima kama kuna mabadiliko katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa baada ya watu kupata umeme, au tofauti kati ya watu wanaopata umeme mwingi au mdogo,” anasema Jennifer. Vikundi vilivyolengwa viliruhusu wananchi kujadili uzoefu wao binafsi, na kutoa ufahamu wa kina juu ya changamoto zinazohusishwa na ukosefu wa upatikanaji wa umeme wa uhakika, na wa bei nafuu.

Ni kwa namna gani, upatikanaji wa umeme unaathiri ushiriki katika shughuli za kijamii na kisiasa?

Utafiti wa awali wa timu hiyo ulipendekeza kuwa kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme kunasababisha kupungua kwa ushiriki wa kisiasa. Nadharia hii moja ilikuwa kwamba mara tu watu wanapokuwa na teknolojia ya umeme majumbani mwao, wana uwezekano mkubwa wa kukaa nyumbani badala ya kutumia muda katika jamii na kujihusisha na maisha ya kisiasa.

Katika mradi wa sasa, watafiti hawakuzingatia tu upatikanaji wa umeme kwa watu, lakini pia ubora wa usambazaji wa umeme. Pia walipanua ufafanuzi wao wa ‘ushiriki wa kisiasa’ ili kujumuisha shughuli mbalimbali zaidi ya upigaji kura, ikijumuisha aina mpya za ushiriki wa kidijitali.

> ***Kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme... inabadilisha tu jinsi watu wanavyofanya siasa.***

“Utafiti wetu mpya unaonyesha kuwa kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme hakupunguzi ushiriki wa kisiasa, inabadilisha tu jinsi watu wanavyofanya siasa,” anasema Alesha. Wakenya leo wanatumia teknolojia zinazowezeshwa na umeme kujihusisha zaidi na siasa, na wanasiasa sasa pia wanatumia mitandao ya kijamii kuungana na wananchi. Hii ina maana kwamba ushiriki wa kisiasa wa Kenya unabadilika sana kama ushiriki ulivyo badilika maeneo mengine. “Hii haihusu tu hatua ya kaya nchini Kenya,” anasema Lauren. “Takwimu zetu zinaungana na hatua pana zaidi ya pamoja ambayo tunaona kwingineko duniani, ambapo wananchi wanapinga ukosefu wa upatikanaji wa umeme wa uhakika.”

Je, ni athari gani kubwa za upatikanaji wa umeme?

Umeme ni muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi (k.m., kuendesha biashara), elimu (k.m., mwanga wa kusoma jioni na kupata habari) na mawasiliano. Hii ina maana kwamba kaya na biashara zenye upatikanaji wa umeme wa uhakika ziko vizuri zaidi kuliko zisizo na umeme. “Katika zama hizi za kidijitali, hata kaya maskini zina simu ambazo lazima ziwe na chaji,” anaongeza Winnie. Kuwa na umeme nyumbani pia huleta faida za kiafya. Taa za umeme na majiko ya kupikia huondoa uhitaji wa mishumaa, taa za mafuta ya taa na jiko la kuni au la mkaa, ambayo yote hutoa hewa mbaya ndani ambayo inaweza kusababisha shida ya kupumua.

Changamoto ya upatikanaji wa umeme kwa usawa

Dhana ya haki ya nishati imekuwa muhimu duniani kote. “Haki ya nishati inamaanisha kuwa wananchi wote wanapata ubora sawa wa umeme wa bei nafuu,” anasema Christopher. Hata hivyo, kufikia hili si rahisi. Changamoto kubwa ni gharama, kwani ni gharama kubwa sana kupanua miundombinu ya gridi ya taifa ili kumfikia kila mtu hasa vijijini. Kisha ni ghali kuunganisha nyumba au biashara kwenye gridi ya taifa, na ingawa serikali hutoa ruzuku kwa hili, pia kuna gharama ya kutumia umeme, ambayo ni ghali sana kwa kaya nyingi maskini. Kaya ambazo hazijaunganishwa kwenye gridi ya taifa mara nyingi hutegemea mifumo midogo midogo ya umeme wa jua, lakini nyingi haziwezi kumudu malipo ya gharama kubwa ya mikopo kwa makampuni binafsi yanayoendesha miradi ya nishati ya jua.

Haya yote yanamaanisha kwamba wakati Kenya imepata maendeleo makubwa katika upanuzi wa umeme mbadala katika miaka ya hivi karibuni, ukweli ni kwamba idadi kubwa ya watu bado hawawezi kufaidika ipasavyo na maendeleo haya.

Kutana *na timu*

Dkt Elizabeth Baldwin
Profesa Mshirika, Shule ya Serikali na Sera ya Umma, Chuo Kikuu cha Arizona, Marekani

Nyanja za utafiti:
Sera ya umma, sera ya mazingira

Nimekuwa nikitamani kufanya kazi katika utumishi wa umma kwa manufaa zaidi. Nilianza elimu yangu ya shahada katika shule ya sheria, lakini haraka nilitambua kwamba ningeweza kuwa na matokeo zaidi kwa kufanya kazi katika sera kuliko ningeweza kutarajia kufikia kwa kumshauri mteja mmoja mmoja kama wakili. Nilipomaliza shule ya sheria, nilipata shahada ya uzamili katika utawala wa umma ikifuatiwa na PhD katika sera ya mazingira. Kwa mafunzo haya, ninaweza kutathmini na kushauri mikakati ya kisera ambayo ni mizuri katika kushughulikia matatizo ya mazingira.

Kuna njia nyingi tofauti za kushiriki katika masuala ya sera. Vijana wanapaswa kujua kwamba sera ya mazingira na nishati ni uwanja unaobadilika - ninajifunza kila mara mambo mapya kuhusu jinsi watu wanavyofanya kazi pamoja kutatua changamoto za sera.

Kama msomi ambaye hutumia muda mwingi afisini kwangu, nilifurahia sana kutoka shambani na kukutana na Wakenya wa kila siku ili kuzungumza kuhusu jinsi wanavyopata umeme, wanavyo utumia na changamoto wanazopitia.

Dkt Jennifer Brass
Profesa Mshirika, Shule ya Masuala ya Umma na Mazingira, Chuo Kikuu cha Indiana, Marekani

Nyanja za utafiti:
Utawala, utoaji wa huduma, NGOs

Baada ya chuo kikuu, nilifanya kazi katika shirika lisilo la kiserikali (NGO) huko Nairobi, Kenya. Uzoefu huu ulinifanya kuzingatia jukumu la serikali na mashirika yasiyo ya faida katika utoaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, huduma za afya na maji safi, na nilishangaa jinsi watu wanavyo chukulia serikali yao wakati wahusika wa kimataifa wasio wa serikali wanatoa huduma hizi. Kwa hivyo, nilisomea PhD katika sayansi ya siasa kutafiti maswali haya.

Ninapenda mchakato wa ugunduzi katika utafiti. Ninauliza maswali ili kuelewa jinsi ulimwengu unavyofanya kazi na mazingira ambayo viwango vya maisha vya watu hupanda. Ili kujibu maswali haya, ninaenda ulimwenguni kuzungumza na watu kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwao. Utafiti huu unaweza kushawishi watunga sera kufanya maamuzi bora.

Hakika ninafurahia sana kuzungumza na Wakenya kuhusu uzoefu wao wa upatikanaji wa umeme. Iwe ni kukutana na maafisa wa serikali ili kujadili mipango ya umeme au kuzungumza na watu wa vijijini ambao hawana umeme, mimi hujifunza zaidi kuhusu matatizo magumu ya usambazaji wa umeme katika mazingira ya kipato cha chini. Ninapenda sana kuweza kuangazia uzoefu wa watu wa kawaida, ambao sauti zao mara nyingi hazisikiki katika mijadala kuhusu upanuzi wa miundombinu.

Dkt Christopher Gore
Profesa, Idara ya Siasa na Utawala wa Umma, Chuo Kikuu cha Toronto Metropolitan, Kanada

Nyanja za utafiti:
Siasa linganishi, nishati na sera ya hali ya hewa

Nilijifunza kuhusu matatizo ya mazingira wakati wa shahada yangu ya kwanza katika sayansi ya mazingira, lakini sikuweza kuelewa kwa nini watu binafsi na serikali hawakujaribu kuboresha hali hizi. Nilivutiwa na ushawishi wa nguvu na mamlaka juu ya mazingira na ustawi wa binadamu, hivyo nikasomea PhD katika sayansi ya siasa na masomo ya mazingira. Nilikuja Afrika Mashariki kwa mara ya kwanza mwaka 2000, ambapo nilijifunza kuhusu viwango vya chini vya upatikanaji wa umeme. Nimekuwa nikijifunza suala hili tangu wakati huo.

Wanasayansi wa siasa hawachunguzi serikali tu; wanachunguza jinsi watu wenye mamlaka wanavyohusiana na wengine katika jamii na jinsi jamii inavyotetea mabadiliko. Ninavutiwa na utafiti wa muktadha ambayo inaweza kuonekana, juu juu, kuwa mibaya au yenye changamoto, lakini, kwa uhalisia, inaonyesha mabadiliko chanya au uthabiti katika nyanja ya utofauti.

Ni fursa ya kujivunia kuzungumza na watumishi wa umma wa Kenya ambao wako tayari kuelezea uzoefu wao kuhusu changamoto zinazozunguka upatikanaji wa umeme. Watumishi wa umma katika nchi za Afrika mara nyingi wanashtumiwa kwa kutofanya kazi kusaidia wananchi. Hata hivyo, nimegundua kuwa watumishi wengi wa umma wanajitolea sana katika kazi zao na wanafanya kazi kwa bidii na rasilimali chache kutafuta ufumbuzi wa changamoto katika nchi zao.

Dkt Lauren MacLean
Profesa, Idara ya Sayansi ya Siasa, Chuo Kikuu cha Kaskazini-Mashariki, Marekani

Nyanja za utafiti:
Idara ya Sayansi ya Siasa, Chuo Kikuu cha Kaskazini-Mashariki, Marekani

Nilishawishika kuwa mwanasayansi ya siasa na mmoja wa maprofesa wangu wa chuo ambaye alianza kila darasa kwa kushirikisha habari muhimu kutoka katika Nchi Zinazoendelea, na kuziunganisha na dhana za sayansi ya siasa. Wakati huo huo, nilijiunga na darasa la Sanaa ya Kiafrika na nikaanza kuona jinsi siasa zilivyowakilishwa katika maisha ya kila siku, na nikashikwa!

Siasa ipo kila mahali! Familia yako, jamii yako, kazi yako, n.k., zote zimeathiriwa na siasa. Sayansi ya siasa ina kufundisha ujuzi wa ajabu wa uchanganuzi ambao unaweza kuutumia ili kutatua tatizo lolote unalokabiliana nalo. Hii inamaanisha kuwa sayansi ya siasa inaweza kukusaidia kufanikiwa katika mipangilio mingi tofauti, kutoka kwa mashirika yasiyo ya faida hadi kwenye makampuni, na kutoka kwa sera ya umma hadi sheria.

Nimejifunza mengi kutokana na kuzungumza ana kwa ana na raia wa Kenya na kusikia kuhusu uzoefu wao wa kile kinachofanya kazi vizuri na kile kinachoweza kuboreshwa kwa siku zijazo. Wametoa mtazamo muhimu ambao unaziba mapengo kutoka kwa mitazamo ya serikali, wafadhili na kampuni zinazofanya kazi kupanua upatikanaji wa umeme.

Dkt Winnie Mitullah
Profesa, Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya

Nyanja za utafiti:
Sera, utawala

Nilizaliwa na kukulia katika jiji la Nairobi, mji mkuu wa Kenya, na nilikua nikihoji aina ya utawala unaohusiana na utoaji wa huduma, hasa kuhusu makazi na ukusanyaji wa takataka. Nilipoenda chuo kikuu, niligundua kuwa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma ilifaa zaidi kusoma nia yangu katika usimamizi wa huduma za umma.

Elimu na taaluma yangu imechangiwa na wasomi walionifundisha wakati wa chuo kikuu na ambao waliniunga mkono wakati wa taaluma yangu ya awali kama msomi mchanga. Pia nilisoma kazi za wasomi wenye msimamo mkali, kama vile Walter Rodney's How Europe Underdeveloped Africa na Ruth First's Barrel of a Gun: Political Power in Africa and the Coup d'État.

Wanasayansi wa siasa hushughulika na masuala ya kiutendaji ya utawala ambayo yanaathiri sekta zote za uchumi. Ninafurahia uwezo wa kuchanganua mienendo ya kisiasa na mabadiliko ya kitaasisi. Kusoma sayansi ya siasa kutajenga uwezo wako wa kujihusisha na hali halisi ya maisha ya kila siku na kukuwezesha kwa majukumu ya ushauri katika viwango tofauti.

Dkt Alesha Porisky
Profesa Msaidizi, Idara ya Sayansi ya Siasa, Chuo Kikuu cha Kaskazini cha Illinois, Marekani

Nyanja za utafiti:
Sera ya kijamii, siasa za Kiafrika

Nilikulia katika familia ya wafanyakazi wa kijamii na, tangu nikiwa na umri mdogo, nimekuwa nikivutiwa na ugumu wa sera ya kijamii na utoaji wa huduma. Wakati wa shahada yangu ya kwanza katika sayansi ya siasa, nilianza kuelewa kwamba swali la 'nani anapata nini, lini na kwa namna ganii?' ni msingi wa kuelewa utekelezaji wa programu za ustawi wa jamii.

Kuna mengi ya kupenda kuhusu kazi katika sayansi ya siasa. Inatoa fursa ya kufikiria juu ya maswali makubwa ambayo yana athari za moja kwa moja kwa maisha ya watu wa kawaida, kutoka kwa nini vita vinapiganwa na jinsi misaada inavyotolewa, jinsi kodi zinavyo tumiwa na namna shule zinavyo endeshwa. Pia ninavutiwa na maswali madogo ya jinsi watu na serikali wanavyo shirikiana, kama vile kujiandikisha kupiga kura au kuhudhuria mikutano ya jumuiya.

Jambo kuu la mradi huu limekuwa ni kizungumza na watu kutoka nyanja mbalimbali kuhusu uzoefu wao juu ya umeme. Mazungumzo haya yameonyesha jinsi umeme ni muhimu kwa ustawi wa kila siku na jinsi ilivyo vigumu kupima 'upatikanaji' wa umeme wa mtu.